

# FOMU YA MKATABA

1. MWAJIRI : WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
CHUO CHA UALIMU MANDAKA  
P.O.BOX ...725...
2. JINA LA FUNDI (mwajiriwa) : MICHAEL KEY MBUGUMBA
3. ENEO LA UJENZI : CHUO CHA UALIMU MANDAKA
4. MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI: LOT 1; BWENI LA WASICHANA  
(Angalia Kiambatisho)
5. GHARAMA YA UFUNDI .....25,605,000..... TZS,
6. MUDA WA MKATABA: Siku 90
7. MASHARTI YA MALIPO: i) Hakuna Malipo ya Awali.  
ii) Fundi atalipwa mara baada ya kazi kukaguliwa.
8. AINA YA MKATABA: Mkataba wa Ufundi
9. MASHARTI YA MKATABA:
  - Mwajiri atatoa Vifaa vya ujenzi atakavyoelekezwa na Mhandisi Mshauri.
  - Fundi atafanya kazi kwa Mujibu wa Mchanganuo wa kazi kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
  - Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kusimamisha kazi na kulipa hasara zote zilizotokana na uzembe au makusudi.
  - Fundi Mkuu atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
  - Fundi Mkuu kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
  - Fundi Mkuu atahusika na vitendo vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake .
  - Fundi Mkuu kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

- Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Mwezi mmoja baada ya kazi kukamilika (Retention Money) nakulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
- Ucheleweshaji wa Kazi:
  - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshaji huo
  - Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri, Fundi ataomba aongezewe muda wa kumaliza kazi.

**NB: Mkataba huu unaweza kuvunjwa mara moja kwa mambo yafuatayo:**

- Iwapo fundi Mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya chuo cha ualimu mandaka.
- Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi wake watafanya kazi bila kufuata mchoro au maelekezo ya Mhandisi Mshauri.
- Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake.
- Ikumbukwe hiki ni chuo chenye vijana wa kike na kiume, hivyo basi Fundi mkuu ahakikishe vibarua wake wanakua na nidham mda wote, lugha za matusi, ulevi kelele, kusimama ovyo na wanachuo, kumletea mwanachuo zawadi yoyote, nakadhalika haviruhusiwi ndani ya eneo la chuo. Fundi mkuu atawajibishwa kwa kusitishwa mkataba wake.

**MWAJIRI:**

Saini: *[Signature]*  
 Jina: TIMOTHEO E. MSANGI  
 Cheo: VICE PRINCIPAL  
 Tarehe: 04-02-2022  
 For, Principal


**MANDAKA TEACHERS COLLEGE**

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: *[Signature]*  
 Jina: Barnabas J. Untala  
 Cheo: Mhandisi Uyenzi  
 Tarehe: 4/02/2022

**FUNDI MKUU:**

Saini: *[Signature]*  
 Jina: Michael Key Mburamba  
 Cheo: Fundi mkuu  
 Tarehe: 4/2/2022



**SHAHIDI WA FUNDI MKUU**

Saini: KUMBWAELY SIMBO  
 Jina: *[Signature]*  
 Cheo: FUNDI  
 Tarehe: 04/02/2022

**KUMBWAELY SIMBO MWASHA**  
 P. O. Box ----- MOSHI  
 TIN. 149 - 054 - 243  
 TEL. 0753 836 863